HOTUBA YA UFUNGUZI WA TAMASHA LA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI ILIYOTOLEWA NA MHESHIMIWA AMANI ABEID KARUME, RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, TAREHE 27 MEI 2010 HOTELI YA BWAWANI.

Waheshimiwa Mawaziri,
Mwenyekiti wa Bodi ya *Foundation for Civil Society*,
Mkurugenzi Mtendaji wa *Foundation for Civil Society*
Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,
Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
Wawakilishi wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali,
Mabibi na Mabwana , Itifaki imezingatiwa

ASSALAM ALAYKUM

Awali ya yote, ninashukuru sana kupata mwaliko huu adhimu wa kufungua maonesho na Tamasha hili la Asasi za Kiraia la mwaka 2010. **Hii ni heshima kubwa mliyonipa mimi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwani hii ni mara ya kwanza kwa kiongozi wa juu wa Serikali ya Mapinduzi kushiriki katika ufunguzi wa Tamasha la Jumuiya Zisizo za Kiserikali Tanzania. Ahsanteni sana.**
Nimearifiwa na waandaaji wa Tamasha na maonesho haya kuwa, Tamasha hili lina malengo makuu manne:

- Kutoa nafasi kwa Jumuiya Zisizo za Kiserikali kujadili na kutafakari nafasi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kukuza ushiriki wa wananchi katika kuimarisha demokrasia, utawala bora na haki za binadamu

- Kusherehekea mafanikio ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali zilizopata ruzuku kutoka *the Foundation for Civil Society* kwa kutambua na kuthamini mafanikio yao hasa zile Jumuiya Zisizo za Kiserikali zinazofanya vyema katika kazi zao za kuwahudumia wananchi.
- Kuzikutanisha pamoja Jumuiya Zisizo za Kiserikali kwa ajili ya kufahamiana na kubadlishana uzoefu.
- Kukuza taswira njema ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali na namna ambayo *Foundation for Civil Society* inaweza ikaimarisha huduma zake za kuzijengea uwezo Jumuiya hizo kwa Tanzania Bara na Visiwani kwa kutoa ruzuku na huduma za kuimarisha uwezo wa Jumuiya kiutendaji na kiutawala.

Ndugu wana Jumuiya Zisizo za Kiserikali ni furaha kubwa kwangu mimi leo kuona kuwa Tamasha hili linafanyika hapa Zanzibar na ni jukwaa muhimu linalotoa nafasi adhimu ya kuwaleta pamoja zaidi ya wawakilishi 300 wa taasisi mbalimbali na wadau wa maendeleo hapa nchini. Miongoni mwao wakiwemo, wasomi, wawakilishi wa serikali, sekta binafsi na nyinyi wanaJumuiya Zisizo za Kiserikali katika kujadili na kutafakari, nafasi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kukuza demkorasia, kukuza ushiriki wa wananchi katika mchakato mzima wa uchaguzi, kukuza elimu ya uraia na elimu kwa wapiga kura. Napenda kusema kuwa nafasi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika mkutadha uliotajwa ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu. Hongereni sana.

Ndugu mwenyekiti

Nimefurahishwa na kutiwa moyo sana kuona kuwa kauli mbiu ya Tamasha la mwaka huu ambayo ni 'Nafasi ya ***Jumuiya Zisizo za***

Kiserikali katika Kukuza ushiriki wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi mkuu nchini. Hili ni jambo linalozijengea serikali zetu – (Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) sifa njema na matumaini makubwa na napenda kusema kuwa, serikali zote mbili zinathamini sana mchango wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kuimarisha demokrasia kama ilivyobainishwa na mipango yetu ya kitaifa ya utawala bora (National Good Governance Strategic Frameworks 2006). Ni kweli usiofichika kuwa , wananchi , kwa kupitia juhudi zenu wamekuwa wakihusika moja kwa moja katika kushirikiana na serikali yao katika kutumia haki zao za kuchagua na kuchaguliwa. Lakini pia ni sahihi kusema kuwa, juhudi zenu za kutoa elimu ya wapiga kura, kutumia vyombo vya habari na elimu ya uraia imesaidia sana nchi yetu ya Tanzania katika kuweka uwanja sawiya wa ushiriki ulio mpana wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi. Hili ni jambo la kutia moyo na ni vyema likaendelezwa.

Ndugu Mwenyekiti

Napenda kuwathibitishia kuwa Serikali zetu zinatambua nafasi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kuwahamasisha wananchi sio tu kushiriki katika michakato ya ujenzi wa demeokrasia lakini pia kuwafanya wananchi waelewe kwa vizuri zaidi umuhimu wa kutumia haki zao za kidemokrasia. Kwa kutumia uwezo wenu wa kuwa karibu na wananchi, kukubalika kwenu, ushawishi wenu, pengine urahisi wenu wa kupata nyenzo kwa dhima ya kukuza demokrasia na imani mliyojijengea imeweza kuongeza ufahamu wa wanannchi juu ya haki zao na hivyo hata idadi ya wapiga kura imekuwa ikiongezeka. Kwa hivyo, nakuombeni mtumie fursa hii kuendeleza ustadi mlionao na mtaji muhimu wa imani ya wananchi kwenu.

Ndugu Mwenyekiti

Serikali zetu katika harakati za kujiletea maendeleo zimejiwekea malengo kupitia mikakati yake ya MKUZA kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na MKUKUTA kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa mikakati hii kwa kiasi kikubwa unategemea taasisi mbali mbali za serikali na zisizokuwa za kiserikali. Kwa maana hiyo Jumuiya zenu zina nafasi na wajibu mkubwa wa kuchangia utekelezaji wa mikakati hiyo. Najua kwamba Jumuiya zenu zinashughulika na utoaji wa huduma mbali mbali, hivyo ni vyema kila wakati mkawa karibu na mipango hiyo.

Ndugu Mwenyekiti

Napenda kusema Tanzania ya kesho iliyo na heshima ya kuwa ni taifa la kidemokrasia lenye kuheshimu misingi ya haki na utawala bora kwa wananchi na viongozi wake inajengwa leo. Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kufikia ndoto hii mnalo jukumu kubwa kwani serikali pekee haiwezi kufanya kila kitu. Huu ni muda muafaka kwenu nyinyi, kwa kutumia jukwaa hili, kutafakari na kujadili kwa kina namna ambavyo wananchi wetu, kwa kutumia taasisi zinazoratibu na kusimamia demokrasia, haki za binadamu na utawala bora nchini zitaweza kutimiza malengo ya kuwa na uchaguzi huru na wa haki, kuongeza ushiriki wa wananchi na kuimarika kwa demkorasia Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa mada zilizotayarishwa (za jumla na somo maalum) zitaibua hamu kubwa kwa washiriki kufahamu na kujenga hamu zaidi ya kuoanisha nadharia na kile kinachotokea. Naelewa kuwa, kuhusika kwenu katika usimamizi na tathmini ya mchakato wa utoaji elimu ya wapiga kura, usimamizi wa uchaguzi, utoaji wa elimu ya uraia kwa chaguzi zilizopita, imewezesha kuibua changamtoto kadhaa ambazo yumkini zikiangaliwa kwa umakini itawezesha kuwa na uchaguzi imara kwa mawaka huu 2010.

Ndugu Mwenyekiti

Ni jambo la kujivunia na inatia moyo kwamba Jumuiya Zisizo za Kiserikali zinao mchango mkubwa sana katika kukuza utawala bora shirikishi na kukuza mustakabali wa maendeleo ya wananchi. Ni imani yangu kuwa mijadala mahsusi inayolenga kuimarisha nafasi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika kukuza demokrasia, utawala bora, haki za kijamii n. k ambayo itawasilishwa kwa siku hizi mbili itajenga hamasa na muamko kwenu nyinyi Jumuiya Zisizo za Kiserikali kuzidi kuwatetea wananchi na katika kuleta fursa sawa na ustawi na haki za kijamii kwa wananchi wote.

Changamoto yangu kwenu wakati mkiendelea na mijadala mbali mbali katika Tamasha na kuonesha kazi zenu kwa umma, napenda mtumie fursa hii mjiulize maswali yafuatato ;

- Kwa kiasi gani mmejihusisha na mchakato wa kuwepo kwa uchagauzi huru na wa haki sambamba na kukuza demokrasia?
- Ni kwa kiasi gani ushiriki wa wananchi katika kukuza haki za binadamu nchini hasa katika kutetea maslahi ya kijamii na kisiasa kwa wananchi, makundi yaliyo pembezoni wakiwemo vijana na wanawake?
- Ni kwa kiasi gani zimesaidia katika kuleta uwazi na uwajibikaji kwa kufanyakazi na vyombo vya habari, taasisi za wanataaluma na kitafiti na wadau wengine?
- Kwa kiasi gani mmeziangalia kasoro zilizomo katika sheria zetu za uchaguzi hapa Tanzania na kupendekeza hatua za marekebisho?

Bila shaka mmefanya kazi kubwa.

Ni matarajio yangu kuwa, mtaandaa mikakati thabiti ya kuyatekeleza kwa vitendo yale yote yatakayotokana na mijadala ya Tamasha hili ili tufike pahala tuseme kuwa sasa tunatembea kifua mbele kwa kuwa na

taifa lenye utawala bora, demkokrasia makini na taifa lenye kuendesha chaguzi huru na za haki kwa mujibu wa vigezo vinavyokubalika kimataifa. Bila shaka tunaweza.

Mabibi na Mabwana

Napenda kutoa wito kupitia Tamasha hili kwenu nyinyi Jumuiya Zisizo za Kiserikali kuwekeza raslimali zenu zaidi katika kuwahudumia ndugu zetu wanaoishi katika mazingira magumu na hasa wale wenye mahitaji maalumu. Hii ina maana kuwa, juhudi zenu za kuimarisha demokrasi, utawala bora na kuhakikisha wigo mpana wa haki za wananchi zilenge katika kuona kuwa watu wanaoishi katika mazingira magumu wanapata haki na fursa zote za kushiriki katika michakato ya uchaguzi. Tathmini za nyuma ambazo nyinyi mmeshiriki katika kuzifanya zimeonesha kuwa, kwa viwango tofauti, makundi hayo yamekuwa hayashiriki kikamilifu katika michakato ya ujenzo wa demokrasia na hasa ile inayohusiana na uchaguzi. Ni matumaini yangu kuwa, Jumuiya Zisizo za Kiserikali mtachukua jukumu la kuongeza ushiriki wa kudumu wa makundi haya katika michakato ya utawala bora, chaguzi mbali mbali na demokrasia shirikishi. Napenda kuona kuwa watu wenye ulemavu, viziwi, bubu, wasioona na wengineo wanashiriki kwa wingi zaidi katika michakato hiyo niliyoitaja. Mahitaji ya makundi haya ndio shabaha ya kuanzishwa Jumuiya za Kiraia na si vyenginevyo.

Mabibi na Mabwana,

Nashawishika kusema kuwa uhusiano wa Jumuiya zenu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali za mitaa umezisaidia sana serikali zetu mbili kujiangalia utendaji wake, kujikosoa na kujifunza kwa dhamira ya kuboresha utendaji wake. Matarajio yangu busara mnazotumia kuziwezesha serikali zetu kujiangalia zingetumika pia katika kuhakikisha kuwa sekta ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali inakuwa mfano wa utawala bora. Hii ni

kutokana na sababu kuwa, utawala Bora sio tu kuinyooshea kidole serikali bali pia hata nyinyi Jumuiya Zisizo za Kiserikali ni vyema mkajiangalia na kujiuliza maswali magumu, je ni kwa kiasi gani mnazingatia demokrasia katika uongozi wenu ndani ya JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI?; Ni kwa kiasi gani mnawajibika kwa walengwa wenu, jamii, serikali, wanachama na wafadhili? Miundo na taratibu zenu zinaruhusu uwazi kwa kiasi gani, chaguzi za viongozi wenu wa Jumuiya ziko huru na ziko wazi kiasi gani? Tukifanya hivyo, ndipo ile dhana ya uwazi, demokrasia na utawala bora shirikishi itaonekana kwa vitendo.

Ndugu Washiriki wa Tamasha, **Mabibi na Mabwana**

Taarifa nyingi za kitafiti na ripoti za ufuatiliaji na tathmini za wadau wa demokrasia na chaguzi mablimbali katika nchi za kusini mwa jangwa la Sahara zinaonesha kuwa tatizo la kuwepo kwa uwezo mdogo wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali kujihusisha katika mchakato wa uangalizi wa uchaguzi na mwenendo wa demokrasia ni changamoto kubwa. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa Jumuiya Zisizo za Kiserikali kuchukua juhudi za makusudi za kujifunza kwa vitendo misingi ya uangalizi wa uchaguzi, kujenga uelewa wa vigezo vya demokrasia, utawala bora na kupima ulinganisho wa hali halisi. Tukifanya hivyo, ndio tutapima na kupata taswira ya hali ilivyo hapa kwetu Tanzania. Nafahamu wapo miongoni mwenu ambao mnachukua juhudi kubwa ya kujifunza na kuzijengea uwezo Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika michakato hiyo. Hongereni sana kwa hilo.

Mwisho, Nawapongeza sana *The Foundation for Civil Society* kwa kuandaa tamasha hili na kuwapongeza pia wawakilishi wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali kutoka Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuweza kukutana pamoja, kufahamiana zaidi, kubadilishana uzoefu na kujenga sekta moja ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali yenye sauti moja na

mwelekeo wa kukuza wigo wa demokrasia, utawal bora n ahali za binadamu Tanzania. .

Baada ya kusema hayo, natamka rasmi kuwa Tamasha la nane la mwaka huu 2010 limefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.